MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA
JARIDA LA HALI YA HEWA

**Na: 33. Msimu wa Kilimo 2018/19 Tathmini ya Kipindi cha Agosti 11-20, 2019 na Matazamio kwa Kipindi cha Agosti 21-31, 2019**

**Muhtasari**


- Mvua za nje ya msimu zinazotarajiwa katika maeneo machache ya ukanda wa ziwa Viktoria, nyanda za juu kaskazini mashariki na Pwani ya kusini na hazitakuwa na manufaa kwa mazao ya msimu.
- Upungufu wa maji na malisho unatarajiwa kuendelea kuongezeka katika maeneo mengi ya nchi kutokana na hali ya ukavu na upepo.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA AGOSTI 11-20, 2019

Katika kipindi cha siku kumi zilizopita, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo eneo la kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kuimarika wakati ile iliyopo eneo la kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) ilipungua nguvu, hivyo kusababisha vipindi vya upepo mkali katika ukanda wote wa pwani. Ukanda wa mvua(ITCZ) uliendelea kubaki kaskazini zaidi mwa nchi.Katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi joto la bahari lilikuwa juu kidogo ya wasttani na kusababisha mvua nyepesi katika maeneo ya ukanda wa pwani. Hata hivyo, uwepo wa mkondo wa mgandamizo mkubwa wa hewa wa Afrika mashariki uliendelea kusababisha vipindi vya upepo mkali uliovuma kutoka kusini hadi kusini mashariki katika ukanda wa pwani yote.

## MWENENDO WA MVUA KATIKA KIPINDI CHA AGOSTI 11-20, 2019

Kwa kipindi hicho maeneo mengi ya nchi yalikua makavu isipokua kwa baadhi ya maeneo machache ya ziwa Victoria hususan magharibi na mashariki mwa ziwa Viktoria ambayo yamepata vipindi vya mvua zilizoambatana na ngurumo . Kiasi cha mvua kilichopimwa ni kati ya 0 mm hadi 10 mm kama inavyojieleza katita kielelezo.




Kielelezo: Kiasi cha mvua katika kipindi cha Agosti 11- 20, 2019

## TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA AGOSTI 11-20, 2019

Katika dikadi hii kwa maeneo mengi yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka hakuna shughuli za kilimo zilizoripotiwa isipokuwa kwa maeneo machache ya nyanda za juu kusini magharibi hususan mkoa wa Mbeya ambapo wakulima walikuwa wanamalizia uvunaji wa mahindi, ngano na maharagwe na mikoa ya kusini hususani mkoa wa Mtwara wakulima walikuwa wanajiandaa na uvunaji wa korosho. Kwa maeneo mengi yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka wakulima wamejihusisha zaidi na ukaushaji wa mazao na kujipanga kwa msimu ujao wa mvua za vuli. Kiasi cha maji na malisho kwa ajili ya mifugo viliendelea kupungua kutokana na hali ya ukavu na upepo.

## HALI YA MAJI ILIVYOKUWA KATIKA KIPINDI CHA AGOSTI 11-20, 2019

Kina cha maji na mtiririko wa maji kwenye mito viliendelea kupungua kiasi kwa maeneo mengi ya nchi kutokana na hali ya ukavu na upepo iliyojitokeza.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA AGOSTI 21-31, 2019

Katika siku kumi zijazo za mwezi, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo eneo la kusini mwa dunia inatarajiwa kuendelea kuimarika wakati ile iliyopo eneo la kaskazini mwa dunia inatarajiwa kupungua nguvu, hivyo kusababisha vipindi vya upepo mkali katika ukanda wote wa pwani. Ukanda wa mvua(ITCZ) unatarajiwa kuendelea kubaki kaskazini zaidi mwa nchi. Joto la bahari la juu kidogo ya wastani linatarajiwa katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi. Hivyo kusababisha mvua katika maeneo ya ukanda wa pwani. Aidha, joto la bahari la juu kidogo ya wastani linatarajiwa katika maeneo ya pwani ya Angola. Hata hivyo uwepo wa mkondo wa mgandamizo mkubwa wa hewa wa Afrika mashariki unatarajiwa kuendelea kusababisha vipindi vya upepo mkali utakaovuma kutoka kusini hadi kusini mashariki katika ukanda wa pwani yote.

## HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA AGOSTI 21-31, 2019

Maeneo ya kanda ya ziwa Victoria (mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara) yanatarajiwa kupata vipindi vifupi vya mvua na ngurumo katika maeneo machache.

Nyanda za juu kaskazini mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro), Pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi) na

Pwani ya kaskazini (mikoa ya Tanga, maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba) yanatarajiwa kupata vipindi vifupi vya mvua katika maeneo machache.

Magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora), kanda ya kati (mikoa ya Dodoma na Singida), nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa) na kanda ya kusini (mkoa wa Ruvuma na maeneo ya kusini mwa Morogoro) yanatarajiwa kuwa na mawingu kiasi.

## MATARAJIO NA USHAURI KWA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA AGOSTI 21-31,2019

Mvua za nje ya msimu zinazotarajiwa katika baadhi ya maeneo nchini hazitakuwa na manufaa kwa mazao ya msimu zaidi zitaathiri mazao ambayo hayajahifadhiwa vizuri na yale ambayo bado yako mashambani. Wakulima wanashauriwa kuhifadhi vizuri mazao ili kupunguza uharibifu wa mazao unaoweza kujitokeza. Hali ya ukavu na upepo inayotarajiwa itapelekea kupungua kiasi kwa maji. Wafugaji wanashauriwa kuwa na matumizi mazuri ya maji yaliyopo na kufuata ushauri unaotolewa na maafisa ugani.

## HALI YA MAJI INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA AGOSTI 21-31, 2019.

Kina cha maji na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuendelea kupungua kiasi kutokana na hali ya ukavu na upepo inayoendelea kujitokeza. Watumiaji wa maji wanashauriwa kuwa na matumizi endelevu ya maji yaliyopo.

*Jarida limetayarishwa na:*

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania
Ghorofa ya 3 -Ubungo Plaza – Barabara ya Morogoro, Dar es Salaam-Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

*S.L.P 3056; Simu. 255 -(0) 22 – 2460706-8; Nukushi: 255 - (0) 22 – 2460718 ; Barua pepe: (1) met@meteo.go.tz (2) agromet@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz*